**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 15 Juni, 2021**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

143. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wigwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Suala la vyeti visivyohalali ni tatizo sugu ambalo limewakumba wananchi walio wengi ndani ya Wilaya ya Micheweni.

(a) Je, Wizara inalijua jambo hili.

(b) Je, ni sababu gani zinazopelekea cheti kuwa sio halali ukizingatia utoaji wa cheti kile kimetolewa na Wizara au Mamlaka husika na kimetiwa saini na Kiongozi mwenye mamlaka hayo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

187. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO katika malengo yake ya mwaka 2020/2021 ilikusudia kuanza ujenzi wa kiwanda cha usarifu wa minofu ya samaki, kuimarisha miundombinu ya baridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki pamoja na kusimamia ujenzi wa chelezo kwa ajili ya maegesho ya boti za ZAFICO.

(a) Je, malengo hayo unayafahamu.

(b) Je, utekelezaji wake mpaka sasa ukoje.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

48. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika juhudi za kuongeza kipato cha mkulima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa punguzo kubwa la bei za pembejeo za kilimo ikiwemo dawa za kuulia wadudu na magugu pamoja na mbolea. Hata hivyo, kumekuwa na ugumu kwa wakulima wa kawaida kuzipata pembejeo hizo hali inayowapelekea kuzinunua kwa bei ya juu au kushindwa kuzinunua kabisa.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuliondosha tatizo hilo.

(b) Je, wakulima wa Zanzibar wanahitaji tani ngapi za mbolea.

(c) Je, Serikali imeagizia tani ngapi za mbolea kwa mwaka.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

25. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Nchi yetu ya Zanzibar kwa kiasi kikubwa inakabiliwa na janga la maradhi yasiyo ya kuambukiza kama vile shinikizo la damu na kisukari. Kwa kuwa mazoezi ya viungo yanasadikiwa kupunguza makali ya maradhi hayo na kwa kiasi kikubwa Serikali imefanikiwa kuyahamasisha maeneo ya mjini  na hatimae kumeanzishwa vikundi vya mazoezi kwa ajili ya kuweka miili sawa na kupunguza athari ya magonjwa haya nyemelezi.

Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu mzuri wa kuratibu vikundi vya mazoezi vijijini hususan katika maeneo ya Kojani, Chwale na Mchangamdogo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

93. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Kwa nini muda umekuwa mkubwa kwa walimu kutolipwa nauli zao.

(b) Je, ni lini walimu hao watalipwa nauli zao na utaratibu gani utatumika katika malipo hayo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

105. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Makoba kiongwe iliahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami na Mhe. Rais mstaafu Dkt Ali Mohamed Shein lakini hadi anaondoka madarakani barabara hiyo haikujengwa. Aidha, Mhe. Rais aliyeko madarakani Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika Mkutano wa Kampeni nae pia aliahidi kujengwa barabara hiyo.

(a) Kwa vile ahadi za viongozi wawili zimekutana, tutarajie nini wananchi wa Makoba Kiongwe.

(b) Kwa kuwa barabara hii imezidi kuwa mbovu na haipitiki, ni lini itajengwa.

142. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara zetu nyingi zinazojengwa na watalamu wetu wa ndani wa Serikali zimekuwa na tatizo kubwa la upasukaji wa barabara hizo na kupelekea mafundi kila siku kutia viraka.

Je, ni lini Wizara itafanya utafiti wa kina kujua chanzo ili kuepuka kujirejea matatizo haya ya ujenzi wa barabara hizo kila muda.

144. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali inaendelea kufanya juhudi mbali mbali za kuendelea kuzijenga barabara za Unguja na Pemba kupitia kampuni mbali mbali za ujenzi.

(a) Je, ni vigezo vipi vinavyochukuliwa na Serikali kuwapatia Wakandarasi hao wa Ujenzi wa barabara hizo.

(b) Je, Wizara haioni kuwa vigezo hivyo vinastahiki kuboreshwa zaidi ili kuendana na wakati.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**

**15 Juni, 2021.** **<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**